# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## WIZARA YA AFYA

**Pitia**: www.lichas.ac.tz Inst: lindi.college.of.health

Namba ya simu**: 0232202295**

**Email:**principal.lindicotc@afya.go.tz**Fax: 0232202295**

Chuo Cha Afya na Sayansi Shirikishi-**Lindi**

S. L. P 278

**LINDI**

**Kumb Na: HE/COTCL/C.9/ 1341** 15/07/2025

**YAH: KUCHAGULIWA KUJIUNGA NA MAFUNZO YA STASHAHADA YA UTABIBU KWA MWAKA WA MASOMO 2025/2026**

Napenda kuchukua nafasi hii kukupongeza na kukutaarifu kwamba Wizara ya Afya kwa kushirikiana na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (NACTVET) imekuchagua kujiunga na mafunzo ya Stashahada ya **Utabibu** ngazi ya Nne (NTA Level 4) katika Chuo cha **AFYA NA SAYANSI SHIRIKISHI-LINDI** Mafunzo haya ni ya miaka mitatu (3).

Chuo kitafunguliwa tarehe **03 Novemba, 2025** na unapaswa kuripoti chuoni kuanzia saa 1.30 asubuhi hadi saa 11.30 jioni. Endapo utashindwa kuripoti ndani ya wiki mbili tangu chuo kufunguliwa nafasi yako itapotea na kujazwa na muombaji mwingine.

Ili kukamilisha usajili na kupokelewa chuoni unatakiwa kufanya yafuatayo: -

i) Kukamilisha malipo ya ada kama ilivyoainishwa katika majedwali ya gharama za mafunzo hapo chini (*Sehemu A*). Malipo haya yatafanyika kupitia benki na mitandao ya simu kwa kutumia namba ya kumbukumbu ya malipo (control number**)** utakayopewa kabla ya kuwasili chuoni. Ili kupata namba ya kumbukumbu malipo, tafadhali wasiliana na Mhasibu wa Chuo kupitia namba ya simu **0715 009 778-GIGWA MBAGA** au **0712 495 386-DR.A.Y.MPILI** Mwanafunzi ambaye hatalipa ada iliyoainishwa kwenye kipengele hicho hatapokelewa.

ii) Pima afya yako katika hospitali (sio zahanati/kituo cha afya) inayotambulika na kujaziwa Fomu ya Matibabu (Medical Examination Form) kabla ya kuripoti chuoni.

iii) Kujaza Fomu ya Uthibitisho wa Utii wa Sheria na Taratibu za Chuo utakayopewa ufikapo chuoni. Unakumbushwa kuzisoma na kuzielewa sheria zote kabla ya kusaini.

iv) Kujaza Fomu iliyoambatishwa hapo chini inayohusu Taarifa za Wazazi/Walezi wako

v) Kununua vifaa vyote vilivyoainishwa katika sehemu B hapo chini vitakavyokuwezesha katika mafunzo yako uwapo chuoni. Hii ni pamoja na sare za chuo.

## SEHEMU A: MAELEKEZO YA MALIPO

Kila mwanafunzi atapaswa kulipa Jumla ya **Tsh 985,400.00 (shilingi laki tisa elfu themanini na tano na mia nne tu)** kwa mwaka (kwa wasio na BIMA ya Afya) na **Tsh 935,000.00 (shilingi laki tisa na elfu thelathini na tano tu)** kwa mwaka kwa walio na BIMA ya Afya kama gharama za mafunzo chuoni. **Fedha hizo zikishalipwa hazirudishwi (non-refundable).**

Mchanganuo wa malipo ni kama ulivyoainishwa katika majedwali yafuatayo:

### I. Gharama zinazolipwa moja kwa moja Chuoni:

Malipo ya vipengele vifuatavyo yatalipwa moja kwa moja chuoni kwa kutumia namba ya kumbukumbu ya malipo (control number**)** itakayotolewa kwa kila mwanafunzi kupitia ofisi ya uhasibu ya chuo. Mwanafunzi anaweza kulipa malipo ya ada ya mwaka mzima kwa mara moja au kwa awamu mbili kama inavyoonekana katika mchanganuo ufuatao:

| KIPENGELE | MALIPO MUHULA WA KWANZA | MALIPO MUHULA WA PILI | JUMLA |
|---|---|---|---|
| Mafunzo | 200,000.00 | 200,000.00 | 400,000.00 |
| Mitihani ya Ndani | 50,000.00 | 50,000.00 | 100,000.00 |
| Usajili | 20,000.00 | - | 20,000.00 |
| Michezo | 10,000.00 | - | 10,000.00 |
| Fedha ya Dharura | 10,000.00 | - | 10,000.00 |
| Malazi (kwa wanafunzi wa bweni) | 75,000.00 | 75,000.00 | 150,000.00 |
| Practicum Guide, Practicum placement fee and Procedure Book | 80,000.00 | - | 80,000.00 |
| **JUMLA** | **445,000.00** | **325,000.00** | **770,000.00** |

**NB: 1. Malipo tajwa hapo juu yanapaswa kufanyika kila mwaka wa masomo. Ada ya muhula wa kwanza italipwa yote mara tu unapowasili chuoni na ya muhula wa pili italipwa ndani ya siku 14 baada ya kuanza muhula wa pili.**

**II. Malipo ya Gharama za Mitihani ya Kitaifa, NACTVET na BIMA ya Afya (NHIF)**

Malipo ya vipengele vifuatavyo yatafanyika pia kwa kutumia namba ya kumbukumbu ya malipo (control number**)** itakayotolewa kwa kila mwanafunzi kupitia ofisi ya uhasibu ya chuo. Ikumbukwe pia kuwa malipo ya vipengele hivi yatafanyika mwanzoni mwa kila mwaka wa masomo.

| **KIPENGELE** | **KIWANGO CHA MALIPO** |
|---|---|
| Gharama za Matibabu (kwa wasio na BIMA) | 50,400.00 |
| Mitihani ya Kitaifa | 150,000.00 |
| NACTEVET Quality Assurance | 20,000.00 |
| **JUMLA** | **220,400.00** |

**NB: Kuwa na Bima ya Afya ni lazima kwa kila mwanafunzi. Ni wajibu wa kila mzazi/mlezi kuhakikisha mwanafunzi anakuwa na Bima ya Afya wakati wa kusajiliwa chuoni au kufanya malipo wakati wa usajili. Mwanafunzi ambaye hatazingatia maelekezo haya hatapokelewa chuoni.**

**SEHEMU B: MAHITAJI YA MWANAFUNZI AWAPO CHUONI**

Yafuatayo ni mahitaji muhimu ambayo mzazi/mlezi utapaswa kumuandalia mwanafunzi kabla ya kufika chuoni.

**I. SARE:**

**Wasichana:** Magauni mawili (2) meupe ya mikono mifupi na urefu unaopita magoti anapokuwa ameketi; magauni hayo yasiwe na ribbon/urembo. Viatu vya Ngozi vyenye rangi vyeusi visivyo na urembo wowote vyenye kisigino kifupi kisichotoa sauti wakati wa kutembea sakafuni na soksi nyeupe, makoti mawili (2) meupe (ya mikono mirefu). Nguo maalum kwa ajili ya kuvaa chumba cha upasuaji (theatre scrubs) rangi ya blue/kijani.
**(**Gharama ya sare ni Tsh **170,000**, Magauni mawili (2) meupe, makoti mawili(2)na sare ya ijumaa ambayo ni Tshirt m o j a na sketi nyeusi moja (1) vyote vinapatikana chuoni)

**Wavulana**: Suruali mbili (2) za kitambaa cha rangi ya khaki (isiwe "cardet" au "jeans"), mashati mawili yenye rangi nyeupe yenye mikono mifupi na yasiyo na urembo wowote au rangi nyingine na vifungo viwe vyeupe au rangi ya maji. Viatu vya ngozi vyenye rangi nyeusi visivyotoa sauti wakati wa kutembea sakafuni na soksi nyeupe na mkanda mweusi wa ngozi.
Makot (2) meupe (ya mikono mirefu). Nguo maalum kwa ajili ya kuvaa chumba cha upasuaji (theatre scrubs) rangi ya blue/kijani.
**(**Gharama ya sare Tsh **170,000**, Suruali Mbili (2) za rangi ya khaki, mashati (2), na sare ya ijumaa ambayo ni Tshirt na suruali nyeusi vyote vinapatikana chuoni)

.
Mara utakapofika chuoni utapewa mwongozo wa mavazi utakaozingatiwa wakati wote uwapo masomoni.

## I. VIFAA SAIDIZI KWAAJILI YA MWANAFUNZI

a) Kifaa cha kupimia mapigo ya moyo (Stethoscope)
b) Kifaa cha kupimia msukumo wa Damu (BP Machine)
c) Kifaa cha kupimia joto la mwili (Thermometer)
d) Kifaa vya kupimia urefu (tape measure)
e) 'Patella Hammer'
f) Tochi ndogo maalumu ya kupimia wagonjwa
***NB Vifaa tajwa hapo juu(a-f) vya kujifunzia vinapatikana chuoni kwa gharama ya Tsh 90,000/=***
g) Vitabu vya rejea vya kozi husika utakavyoelekezwa baada ya kufika chuoni.
h) Vifaa vya kuandikia kwa mfano madaftari, kalamu, rula n.k
i) Nguo na viatu vya michezo mbali mbali.
j) Ndoo kubwa ya plastiki (ujazo wa lita 20) ya kutunzia maji.
k) Godoro (urefu wa futi tatu kwa sita)
l) Mwamvuli au koti la mvua
m) Shuka nne (4) zenye rangi ya *light blue* kwa wavulana na *pink* kwa wasichana, mto mmoja na foronya mbili zenye rangi ya shuka, blanketi moja (1), chandarua na taulo.
n) Mwanafunzi aje na computer mpakato (laptop) ili kurahisisha kujifunza

## II. VIFAA SAIDIZI KWA AJILI YA CHUO

a) Ream‟ moja ya karatasi ya kutolea nakala/kudurufu (photocopy) kwa kila muhula kwa wanafunzi wanaoanza na wanaoendelea. (aina ream zilizopendekezwa ni Paperline, . Ream tofauti na hizo hazitapokelewa)
b) Sabuni ya maji yenye ujazo wa Lita tano.
c) ARO Chupa moja (1) yenye ujazo wa lita (1)
d) Picha nne (4) Passport size.
NB vifaa tajwa hapo juu vinapatikan chuoni

Ninakutakia masomo mema.

…………………………………………….
**MKUU WA CHUO**

**KIAMBATISHO I: Fomu ya Uthibitisho wa Utii wa Sheria na Taratibu za Chuo**

**Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**

**Wizara ya Afya**

**Idara ya Mafunzo na Maendeleo ya Wataalam**

**Fomu ya uthibitisho wa utii wa Sheria na taratibu za chuo kwa wanafunzi waliochaguliwa kujiunga na masomo ya afya kwa ngazi za stashahada**

**Jina la Chuo: CHUO CHA AFYA NA SAYANSI SHIRIKISHI-LINDI**

**Mwaka wa Masomo: 2023/2024**

**Kozi: STASHAHADA YA UTABIBU**

## SEHEMU A: SHERIA NA TARATIBU ZA CHUO

1. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa katika mazingira ya shule ifikapo saa 2.00 usiku. Mwanafunzi atakayekuwa nje ya chuo zaidi ya muda uliotajwa hapo juu kwa sababu maalum anatakiwa kupata ruhusa maalum kwa maandishi (gate pass) toka kwa Mkuu wa chuo au Mlezi wa chuo.
2. Kila mwanafunzi atawajibika kwa usafi wa chumba anachoishi na usafi wa mazingira ya chuo.
3. Hairuhusiwi kubandika magazeti/vipande vya magazeti au picha kwenye kuta za majengo ya chuo.
4. Kila mwanafunzi atatakiwa kushiriki kikamilifu katika michezo na shughuli nyingine za chuo kama zitakavyoelekezwa na uongozi wa chuo.
5. Wageni hawaruhusiwi kuingia kwenye eneo la chuo bila idhini ya mlezi au Mkuu wa Chuo. Endapo mgeni/wageni watahitaji kuzunguka na kuangalia maeneo ya chuo, watatakiwa kupata kibali toka kwa Mkuu wa chuo.
6. Wageni hawaruhusiwi kuonana na wanafunzi wakati wa masomo na wanatakiwa kuwa wameondoka kwenye maeneo ya chuo ifikapo saa 12 jioni

7. **Wageni wote wanaoingia chuoni kuona wanafunzi wanatakiwa kuripoti kwa mkuu wa chuo/mlezi wa wanafunzi kabla ya kuonana na mwanafunzi, kuandikisha katika kitabu cha wageni kinachoonesha jina la mgeni, mahali anakotoka, uhusiano na mwanafunzi anayemtembelea, anuani yake na muda wa kuingia na kutoka. Mwanafunzi atakayekutwa akiwa na mgeni kwenye eneo la chuo bila taarifa atachukuliwa hatua za kinidhamu.**
8. Hairuhusiwi wanafunzi wa kiume kwenda kwenye mabweni ya wanafunzi wa kike na vivyo hivyo kwa wanafunzi wa kike kwenda kwenye mabweni ya wanafunzi wa kiume.
9. Wanafunzi wanatakiwa kuvaa sare za chuo zenye staha wakati wote wanapokuwa darasani, katika mafunzo kwa vitendo hospitalini na shughuli nyingine za chuo kama itakavyoelekezwa na uongozi wa chuo.
10. Matumizi ya pombe, sigara, madawa ya kulevya hayaruhusiwi mwanafunzi anapokuwa masomoni. Mwanafunzi atakayebainika kutumia atakuwa amevunja sheria na hivyo kuchukuliwa hatua.
11. Upigaji wa kelele katika maeneo ya chuo au hospitali hauruhusiwi.
12. Wanafunzi wote wanawajibika kutunza vifaa na majengo ya chuo. Ni marufuku kujihusisha na uharibifu wa aina yeyote. Aidha, mwanafunzi atakayeharibu mali ya chuo, atawajibika kuilipa pamoja na kuchukuliwa hatua za kinidhamu.
13. Hairuhusiwi kukaa na silaha ya aina yeyote, ikiwemo kisu au panga.
14. Mwanafunzi yeyote mwenye vifaa vya umeme mdogo kama kompyuta, radio ndogo na pasi, atoe taarifa kwa Mkuu wa Chuo. Aidha, mwanafunzi haruhusiwi kuwa na jiko la aina yoyote au kifaa chochote cha kuchemshia maji (heater) katika eneo la chuo.
15. Mwanafunzi anayeumwa anatakiwa kutoa taarifa kwa Mkuu/Mlezi wa Chuo. Kila mwanafunzi anayehudhuria matibabu awe na ‘sick-sheet’ kabla ya kupata matibabu isipokuwa pale tu matibabu yake yanakuwa ya dharura na upatikanaji wa ‘sick-sheet’ ni mgumu. Hata hivyo, bado mwanafunzi huyo atatakiwa kujaziwa ‘sick-sheet’ wakati au baada ya matibabu. ‘Sick-sheet’ zote zinatakiwa kurudishwa kwa Mkuu/Mlezi wa chuo na kutunzwa kwenye majalada ya kumbukumbu za wanafunzi husika.
16. Mwanafunzi yeyote atakayethibitika kushiriki kutenda kosa la jinai atafukuzwa chuo.
17. Mwanafunzi anatakiwa kushiriki kikamilifu katika matukio yote yanayohusu mafunzo bila kukosa. Ni marufuku kwa mwanafunzi kuondoka eneo la chuo/mafunzo bila taarifa ya maandishi kutoka kwa mkuu wa chuo/mlezi wa wanafunzi.
18. Mwanafunzi haruhusiwi kutumia lugha ya matusi au udhalilishaji, kupigana, kufanya migomo, kushiriki vikao ambavyo sio rasmi, kuandamana kinyume cha utaratibu, kuiba na kumiliki mali kinyume cha sheria.
19. Mwanafunzi haruhusiwi kufanya vitendo vyenye kushawishi ngono ndani ya mazingira ya chuo na hospitali
20. Mwanafunzi anaruhusiwa kushiriki hafla za kiimani zinazohusiana na imani ya dini mbalimbali baada ya kuwa amepata kibali kutoka kwa Mkuu wa Chuo. Aidha, ushiriki wa shughuli yoyote ya kidini itakayothibitika kuingilia ratiba ya mafunzo au uvunjifu wa amani hautaruhusiwa.
21. Mwanafunzi haruhusiwi kushiriki au kuendesha harakati za kisiasa chuoni
22. Mwanafunzi atakayedhihirika kuwa mjamzito hataweza kuendelea na masomo. Atarudishwa nyumbani mpaka ajifungue na kulea mtoto kwa miezi isiyopungua sita. Kisha atapewa utaratibu wa kurejea na kuendelea na masomo.
23. Mwanafunzi anatakiwa kufuata taratibu zote wakati wa mitihani. Aidha kushiriki katika kughushi matokeo ya mitihani, nyaraka za serikali hakutavumiliwa, na hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi ya wahusika.

**SEHEMU B: MWONGOZO WA MAVAZI**

**1. NGUO ZINAZORUHUSIWA**

Ili kurahisisha usimamizi wa mwongozo huu vyuoni na pia ili kuwasaidia wanafunzi waweze kufanya kilicho sahihi, ufafanuzi wa nguo zinazoruhusiwa ni kama ifuatavyo:

***1.1 Kwa wasichana/wanawake***

a) Wavae sketi au gauni isiyo ya kubana, kitambaa kisichokuwa *transparent* na iwe ndefu ya kuvuka magoti akiwa amekaa
b) Kuvaa sare pamoja na vitambulisho wakati wote wa darasa, wodini na maeneo ya mazoezi kwa vitendo nje ya chuo
c) Sare:
   - Sare za wauguzi: Wavae gauni ya mikono mifupi yenye rangi na mtindo uliochaguliwa na Baraza la Uuguzi na Ukunga.
   - Sare kwa kada za vyuo vya Sayansi Shirikishi: Gauni nyeupe ya mikono mifupi isiyokuwa na ribbon
d) Nguo zilizoruhusiwa katika maeneo ya mazoezi kwa vitendo (mfano; koti jeupe)
e) Nguo safi na zilizopigwa pasi
f) Nguo za michezo na tisheti zilizochaguliwa na taasisi/ serikali ya wanafunzi
g) Uvaaji wa soksi ndefu za aina moja zenye rangi nyeupe
h) Hijabu iwe ya rangi nyeupe na iwe fupi inayoingizwa kwenye sare

***1.2 Kwa wavulana/wanaume***

a) Kuvaa suruali ndefu zisizo za kubana na kuchomekea na kufunga mkanda pamoja na kuvaa vitambulisho wakati wote wa darasani, wodini na maeneo ya mazoezi kwa vitendo nje ya chuo
b) Sare:
   - Sare za wauguzi: Wavae shati na suruali yenye rangi na mtindo uliochaguliwa na Baraza la Uuguzi na Ukunga.
   - Sare kwa kada za vyuo vya Sayansi Shirikishi: Suruali ya khaki na shati jeupe lenye mikono mifupi.
c) Nguo zilizoruhusiwa katika maeneo ya mazoezi kwa vitendo (mfano; koti jeupe)
d) Nguo safi zilizopigwa pasi
e) Nguo zinazoendana na rangi iliyochaguliwa na taasisi/Baraza la taaluma
f) Nguo zenye mtindo wa kushona uliopitishwa na taasisi/Baraza la taaluma
g) Nguo za michezo na tisheti zilizochaguliwa na taasisi/ serikali ya wanafunzi
h) Uvaaji wa soksi za aina moja zenye rangi nyeupe
i) Vest au T-Shirt inayovaliwa ndani ya shati iwe yenye rangi nyeupe

**1.3 Nguo za kujikinga na baridi zinazoruhusiwa kwa jinsia zote**

*a)* Sweta lenye rangi nyeupe lisilokuwa na urembo au maandishi yeyote.
*b)* Kwa vyuo vilivyoko kwenye mikoa yenye baridi kali wanafunzi wanaruhusiwa kuvaa mavazi ya nyongeza juu ya sare ya chuo mfano skafu nyeupe na koti lenye rangi nyeupe

## 2. NYWELE ZINAZORUHUSIWA

Ili kurahisisha usimamizi wa mwongozo huu vyuoni na pia ili kuwasaidia wanafunzi waweze kufanya kilicho sahihi, ufafanuzi wa mitindo ya nywele inayoruhusiwa ni kama ifuatavyo:

***2.1 Kwa wasischana/wanawake***

a) Nywele fupi za asili za kuchania kitana

b) Nywele ndefu za asili zifungwe kwa vibanio kuelekea kisogoni ili sura ionekane na zisiachwe kuning’inia

c) Nywele za asili za kusuka kwa msitari bila rasta (*Utii wa Rhoda*)

***2.2 Kwa wavulana/ wanaume***

a) Nywele fupi za asili zinazolingana za kuchania kitana

## 3. UREMBO UNAORUHUSIWA

Ili kurahisisha usimamizi wa mwongozo huu vyuoni na ili kuwasaidia wanafunzi waweze kufanya kilicho sahihi, ufafanuzi wa aina ya urembo unaoruhusiwa ni kama ifuatavyo: a) Pete za ndoa b) Kucha fupi

c) Saa

d) Miwani kwa wenye matatizo ya macho

e) Kofia kwa wenye matatizo ya ngozi (Albino)

## 4. VIATU VINAVYORUHUSIWA

Ili kurahisisha usimamizi wa mwongozo huu vyuoni na ili kuwasaidia wanafunzi waweze kufanya kilicho sahihi, ufafanuzi wa viatu vinavyoruhusiwa ni kama ifuatavyo:

a) Viatu vyeusi vyenye kisigino kifupi kisichotoa sauti wakati wa kutembea sakafuni.

b) Viatu vya michezo wakati wa michezo

## 5. MAVAZI YASIYORUHUSIWA

**5.1 Mavazi yasiyoruhusiwa kwa wasichana/ wanawake**

a) Nguo zinazobana

b) Nguo (gauni/sketi) fupi zinazoacha magoti wazi wazi manafunzi akiwa amekaa.

c) Nguo zinazoacha sehemu ya mwili wazi kama kitovu na kifua

d) Nguo zinazoonyesha maungo/ nguo za ndani (transparent)

e) Nguo zilizokunjamana (Hazikunyooshwa)

f) Nguo chafu (Hazikufuliwa)

g) Nguo zilizochanika/kufumuka zipu au vifungo

h) Nguo zisizoendana na rangi zilizopendekezwa kwenye fomu ya kujiunga chuoni

i) Nguo zisizoendana na mtindo uliopendekezwa kwenye fomu ya kujiunga chuoni

j) Nguo ambazo zina picha, michoro, na maandishi ambayo hayaendani na shughuli za serikali

k) Kaptura aina yoyote ile kama vile pedo na pensi

l) Suruali zilizofumuliwa (zilizotobolewa) kwenye sehemu ya magoti na mapajani

m) Kwenda na khanga/kitenge kwenye bwalo la chakula bila kuwa na nguo ya ndani

n) Kuvaa nguo za kulalia (night dress) kwenye makundi ya kusoma na kupita nazo kwenye mazingira ya chuo

o) Nguo yenye maandishi ya chama chochote cha siasa au ushabiki wa kitu fulani

p) Nguo yoyote inayopingana na maadili ya Utumishi wa Umma

q) T-shirt zenye picha za kutisha na maandishi yasiyo na staha

**5.2 Mavazi yasiyoruhusiwa kwa wavulana/wanaume**

a) Suruali aina ya kadeti au jeans kutumika kama sare (hata kama ni ya rangi ya khaki)
b) Suruali za kubana (modo)
c) Shati la kubana (Slimfit)
d) Kuvaa suruali mlegezo (*Kata K*)
e) Nguo zinazoacha sehemu ya mwili wazi kama kitovu na kifua
f) Kufunga vifungo vichache vya shati ili kifua kionekane
g) Nguo zilizochanika/kufumuka zipu au vifungo
h) Nguo zisizoendana na rangi zilizopendekezwa kwenye fomu ya kujiunga chuoni
i) Nguo zisizoendana na mtindo uliopendekezwa kwenye fomu ya kujiunga chuoni
j) Suruali yoyote fupi au iliyoachwa bila kupindwa chini
k) Suruali zilizofumuliwa (zilizotobolewa) kwenye sehemu ya magoti na mapajani
l) Kaptura ya aina yoyote
m) Nguo yenye maandishi ya chama chochote cha siasa au ushabiki wa kitu fulani
n) Nguo yoyote inayopingana na maadili ya Utumishi wa Umma
o) Nguo ambazo zina picha, michoro, na maandishi ambayo hayaendani na shughuli za serikali

**6. NYWELE ZISIZORUHUSIWA**

a) Nywele chafu ambazo hazikutengenezwa vizuri
b) Nywele bandia au zilizopakwa rangi
c) Kufuga nywele ndefu kwa wavulana/wanaume
d) Kusuka rasta au mtindo wowote wa nywele za kuning'inia
e) Unyoaji nywele mitindo isiyofaa k.m *kiduku, pank, zungu la unga* (kipara)
f) Kufuga ndevu

**7. UREMBO USIORUHUSIWA**

a) Hereni, Bangili, Mikufu, Pete ambazo si za ndoa pamoja na manukato yenye harufu kali
b) Kunyoa nyusi na kupaka wanja
c) Kupaka rangi za midomo
d) Kufuga kucha ndefu
e) Kupaka rangi kwenye kucha
f) Uvaaji wa kucha bandia
g) Meno ya urembo wa dhahabu hayaruhusiwi

**8. VIATU VISIVYORUHUSIWA**

a) Kandambili pamoja na makobazi
b) Viatu vya michezo pamoja na raba (isipokuwa wakati wa shughuli maalum za michezo)
c) Viatu vya rangi isiyopendekezwa kwenye fomu ya kujiunga chuoni
d) Kuvaa viatu bila socks
e) Viatu vya mchuchumio
f) Viatu vya kisigino vyenye kutoa sauti kwenye sakafu

**ANGALIZO:** Uvunjaji wa taratibu zilizoainishwa hapa juu unaendana na adhabu, ambazo zimeelekezwa katika kitabu cha maadili ya wanafunzi walioko katika vyuo vya afya kilichotolewa, na Wizara ya Afya mwaka 2019 (Disciplinary Code for Students in Health Training Institutions Revised 2019)

**SEHEMU C: UTHIBITISHO**

Mimi.......................................................................niliyechaguliwa kujiunga na masomo ya Afya kwa kada ya……………………………………. Ngazi ya …………………………………………..
nathibitisha kuzisoma na kuzielewa Sheria na Taratibu za Chuo pamoja na Mwongozo wa Mavazi niwapo chuoni.
Hivyo nathibitisha kuwa nitakuwa tayari kuzifuata kwa kipindi chote nitakachokuwa hapa chuoni na nakubali kuchukuliwa hatua za kinidhamu endapo nitathibitika kukiuka taratatibu hizo.

Jina la Mwanafunzi: ………………………………………………………………

Sahihi: …………………………………………………………………………….

Tarehe: ……………………………………………………………………………

Mimi .......................................................................Mzazi/Mlezi/Mfadhili wa mwanafunzi tajwa hapo juu aliyechaguliwa kujiunga na masomo ya Afya kwa kada ya……………………………………. ngazi ya ………………………………………….. nathibitisha kuzisoma na kuzielewa Sheria na Taratibu za Chuo pamoja na Mwongozo wa Mavazi utakaozingatiwa na mwanangu awapo chuoni.
Hivyo nathibitisha kuwa nitakuwa tayari na nakubali mwanangu achukuliwe hatua za kinidhamu endapo atakiuka taratatibu hizo.

Jina la Mzazi/Mlezi: ………………………………………………………………

Sahihi: …………………………………………………………………………….

Tarehe: ……………………………………………………………………………

Imepokelewa na kushuhudiwa na:

Jina la Mkuu wa Chuo: ……………………………………………………………

Sahihi: ……………………………………………………………………………..

Tarehe: ……………………………………………

**KIAMBATISHO II: Fomu ya Matibabu**

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**MINISTRY OF HEALTH**

**MEDICAL EXAMINATION FORM FOR STUDENTS JOINING ALLIED HEALTH TRAINING INSTITUTIONS AND NURSING SCHOOLS**

**NAME OF THE INSTITUTION: LINDI COLLEGE OF HEALTH AND ALLIED SCIENCES**

**PROGRAMME: CLINICAL MEDICINE**

**YEAR OF STUDY: 2023/2024**

## PART A: STUDENT'S PARTICULARS

STUDENT'S FULL NAME: …………………………………………………………………..

DATE OF BIRTH: ……………………………………………………………………….

SEX: (Male/Female)………………………MARITAL STATUS: ……………………………..

## PART B: STUDENT'S MEDICAL HISTORY

Does the examinee have current history of any of the following? Indicate ***YES*** or ***NO***

Tuberculosis? ..............................

Epilepsy? ....................................

Sickle cell? ………………………

Asthmatic or with Allergic to something (*specify*)? …………..

Psychiatric? ………………………

Vision impairment? ……………..

Hearing disorder? ……………….

Physical disability? ……………..

Any other significant medical condition/disorder? (*please specify*) …………………………

## PART C: PHYSICAL EXAMINATION

Height (cm): ……………………. Weight (kg): ………………….. BP (mmHg): ………………..

Any significant finding from systemic examinations (*please specify*):

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………

## PART D: INVESTIGATIONS' FINDINGS

Please indicate any significant finding from the following Laboratory and Radiological tests

FBP: …………………………………….. Urinalysis: ………………………………………………

Random Blood Sugar (*provide the results*): ………………………… Blood group ……………….

Stool analysis: ………………………………

Any other relevant investigation performed (*please give brief findings*):

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………….

## PART E: CONCLUSION

I have examined Mr./Miss/Mrs… ..........................................................................................and Consider that he/she is physically and mentally **fit/not fit** to be admitted to the college for studies.

…………………... ...………… ……………………………………..

Name Signature Date

Qualification ……………………… Title ……………………………………….

Hospital's Name: ……………………………………………………………………………..

(*Official hospital's stamp*)

**KIAMBATISHO III: Fomu ya Usajili**

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**

**MINISTRY OF HEALTH**

**INSTITUTION NAME: LINDI COLLEGE OF HEALTH AND ALLIED SCIENCES**

**STUDENT'S REGISTRATION FORM**

| **ADMISSION OFFICE** |
|---|
| |

STUDENT NAME ……………………………………………………………

DATE OF BIRTH …………………………………………………………….

NATIONALITY ………………………………………………………...

ADDRESS …………………………………………………………………

SEX Male: ☐ Female: ☐

MARITAL STATUS …………………………………………………………

TELEPHONE NUMBER …………………………………………………

NACTVET REG NUMBER ………………………………………………

PROGRAM ……………………………………………………………….

NTA LEVEL ………………………………………………………………

REMARKS FROM NACTVET SYSTEM Available: ☐ Not Available: ☐

*If **Not Available**, state why?*

……………………………………………………………………………………......

ADMISSION OFFICER'S SIGNATURE ……………………………………………

## TAARIFA ZA MZAZI/MLEZI

Passport size

**NDUGU WA KWANZA**

JINA KAMILI (MATATU) …………………………………………………………………………………

UHUSIANO NA MWANAFUNZI…………… …………………………………………………...
ANUANI YA POSTA: ………………………………………………………………………………

MTAA: ……………………………KATA: ………………...WILAYA: …………………...

MKOA: ………………………………………NAMBA YA SIMU: ……………………

BARUA PEPE: ……………………………………….

**NDUGU WA PILI**

JINA KAMILI (MATATU) …………………………………………………………………………………

UHUSIANO NA MWANAFUNZI…………… …………………………………………………...
ANUANI YA POSTA: ………………………………………………………………………………

MTAA: ……………………………KATA: ………………...WILAYA: …………………...

MKOA: ………………………………………NAMBA YA SIMU: ……………………

BARUA PEPE: ……………………………………….

Nathibitisha kuwa taarifa nilizojaza hapo juu ni sahihi na kweli tupu.

JINA KAMILI LA MZAZI/MLEZI………………………..……………………………………………

SAHIHI: ……………………………………………. TAREHE:…………………………………………

Imesainiwa mbele ya (Ijazwe na Mtendaji wa Kata/mtaa/Kijiji)

JINA KAMILI ……………………………………………CHEO: ………………………………………..

ANUANI YA POSTA: ………………...……………………………………………………………..

MTAA: ……………………………KATA: ………………..WILAYA: ……………………..

MKOA: ………………………………………NAMBA YA SIMU: ………………………..

SAHIHI: ………………………………. MUHURI WA OFISI: ………………………………

TAREHE: …………………………………………………….

**ACCOUNTANT'S OFFICE (*Payment of School Fees*)**

TOTAL AMOUNT PAID ……………………………………………..

TOTAL AMOUNT NOT PAID ….…………………………………………..

REASON FOR AMOUNT NOT PAID……………………………………………………………………………

PAID SMESTER II EXAMINATION FEES? YES ☐ NO ☐

ACCOUNTANT'S SIGNATURE

……………………………………………..

STUDENT'S SIGNATURE ……………………………………………..

**PATRON / MATRON OFFICE (*if accommodation offered*)**

HOSTEL NAME / BLOCK ……………………………………………..

ASSIGNED ROOM NUMBER ……………………………………………..

STUDENT'S DISABILITY (*Briefly describe in case of any disability*)

……………………………………………..……………………………………………..

……………………………………………..……………………………………………..

……………………………………………..……………………………………………..

PATRON / MATRON SIGNATURE ……………………………………………..

**STUDENT'S DECLARATION**

I ......................................................................... declares that all the information provided are correct to the best of my knowledge and shall be held responsible in case of wrong information.

STUDENT'S SIGNATURE ……………………………………………..

DATE ……………………………………………..

## WIZARA YA AFYA

**KIAMBATISHO NA. IV: FOMU YA MZAZI/MLEZI WA MWANAFUNZI**

1. **Uthibitisho wa Mzazi/Mlezi**

Mimi Bw/Bi/…………………………………………………………………ambaye ni mzazi/mlezi wa Bw/Bi……………………………………………………….…nakiri kupokea maelekezo ya Wizara/Chuo yanayomhusu kijana wangu. Ninaahidi kumsimamia mwanafunzi huyu atekeleze maelekezo yote ikiwa ni pamoja na kulipa ada kwa ukamilifu ili aweze kupokelewa chuoni na kuanza masomo ndani ya muda uliopangwa. Pia ninaahidi kushirikiana na uongozi wa chuo kuhakikisha mwanafunzi huyu anasoma kwa bidii na kuonyesha nidhamu wakati wote wa mafunzo.

Jina kamili la mzazi/mlezi (Wa kiume)……………………………………………………..

Kazi anayofanya: ………………………………………………………………

Anuani kamili: ………………………………………………………………

Namba za simu: ………………………………………………………………

Barua pepe: ………………………………………………………………

Saini: ……………………………………………………………………

WEKA PICHA YA BABA MZAZI/ MLEZI WA KIUME HAPA

Jina kamili la mzazi/mlezi (wa kike)……………………………………………………….

Kazi anayofanya: ………………………………………………………………

Anuani kamili: ………………………………………………………………

Namba za simu: ………………………………………………………………

Barua pepe: ………………………………………………………………

Saini: ……………………………………………………… …………..

WEKA PICHA YA BABA MZAZI/ MLEZI WA KIUME HAPA

**Taarifa ya Mtendaji wa kata**

**Jina la Afisa Mtendaji wa Kata:** ………………..…………………………..………………..

**Jina la kata:** …………………..………………………..……………………………..

**Anuani :** ……………………………………………………………………………….

**Namba za simu:** ……………………………………………………………………………….

**Barua pepe:** ……………………………………………………………………………….

**Saini**: ……………………………………………………………………………….

Muhuri wa ofisi